**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA KILIMO, WIZARA YA FEDHA, NA**

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA**

**9 Aprili 2025**

# TANGAZO LA ZABUNI YA UENDESHAJI WA GHALA ZA MAZAO YA KILIMO TANZANIA

## 1. UTANGULIZI

Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB), Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA), Bodi ya Korosho Tanzania (CBT), Soko la Bidhaa Tanzania (TMX), na Tume ya Ushirikika Tanzania (TCDC) wanakusudia kufanya upekuzi (*vetting)* kwa waendeshaji wa maghala (*warehouse operators*) watakaoruhusiwa kuendesha maghala yatakayotumika kuhifadhi na kuendesha mfumo wa stakabadhi za ghala kwenye mazao yote yanayosimamiwa na Taasisi husika yakiwemo; Korosho, Ufuta, Mbaazi, Dengu, Soya, Choroko na Mengineyo.

Zoezi hili linalenga kutathmini na kubaini waendeshaji ghala wenye sifa stahiki ambao wanaweza kuendesha ghala kwa viwango vinavyohitajika ili kuhakikisha kuna ufanisi, usalama na ubora wa huduma za uhifadhi wa mazao ya kilimo nchini. Pindi zoezi litakapokamilika, waendesha ghala pekee ambao watakidhi vigezo vya upekuzi watatangazwa rasmi na kuruhusiwa kuomba leseni ya uendeshaji ghala kupitia Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za ghala (WRRB) pale fursa inapojitokeza. Aidha, waendesha ghala ambao wana mikataba hai na kushindwa kufikia vigezo vilivyowekwa, mikataba yao itasitishwa mara moja. Taratibu zitafuatwa na taratibu za kutafuta mwendesha ghala mwingine zitafuatwa.

## 2. VIGEZO/SIFA KWA MWOMBAJI

Mwombaji mwenye nia ya kuendesha ghala anatakiwa awe na sifa/vigezo vifuatavyo;

i. Awe na uzoefu usiopungua miaka mitano (5) katika uendeshaji wa ghala la kuhifadhi mazao ya kilimo na kupata daraja linalostahili kwa mujibu wa viwango vilivyowekwa na WRRB. Aidha Kampuni zenye uzoefu wa miaka michache zitafanyiwa upekuzi ili kujiridhisha kuhusu uwezo wao;
ii. Awe na uwezo wa kuhifadhi na kusimamia mazao kwa kuzingatia viwango vya usalama wa chakula na ubora wa mazao;
iii. Awe na nyaraka zinazo onesha uwezo wa kifedha wa kuendesha ghala, ikiwa ni pamoja na kuweka kinga ya dhamana itakayoendana na kiasi cha mazao atakayokuwa anahifadhi. Kiwango cha chini cha dhamana itakayowekwa kwa waendesha ghala kitakua ni fedha Taslim Tsh. 50,000,000 au kulingana na thamani ya zao na ukubwa wa ghala;
iv. Awe na uwezo wa kuwekeza katika miundombinu na teknolojia za kisasa za kuhifadhi mazao kulingana na mahitaji yaliyoainishwa kwenye miongozo mbali mbali ya uhifadhi wa mazao;
v. Awe na mpango wa uendeshaji wa ghala unaoonyesha usimamizi wa hesabu, ufuatiliaji wa bidhaa na hatua za kudhibiti upotevu wa mazao;
vi. Awe na mtumishi mwenye vyeti vya kitaaluma katika masuala ya hifadhi, ubora na usimamizi wa ghala;
vii. Awe na uzoefu wa kushirikiana na taasisi za serikali au sekta binafsi katika uendeshaji wa ghala;
viii. Asiwe na historia mbaya katika shughuli za uendeshaji ghala nchini; na
ix. Awe na sifa nyingine zote zilizowekwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Stakabadhi za ghala.

## 3. UTARATIBU WA KUWASILISHA MAOMBI

Mwombaji mwenye nia ya kuendesha ghala la mazao tajwa anakaribishwa kuwasilisha taarifa zake kwa njia ya maandishi zikijumuisha:

i. Wasifu wa kampuni;
ii. Taarifa za Wakurugenzi wa Makampuni;

iii. Taarifa za menejimenti ikiwemo meneja ghala pamoja na vyeti vyake vya kitaaluma;
iv. Nyaraka za usajili na leseni ya kampuni;
v. Ushahidi wa uzoefu wa uendeshaji ghala;
vi. Ripoti za kifedha na mpango wa uendeshaji wa ghala;
vii. Ushahidi wa uwezo wa kifedha itakayotumika kwenye kinga ya dhamana. (Taarifa za Kibenki ikiwemo dhamana ya benki '*bank guarantee'* ziwe tayari kuwasilishwa zitakapohitajika);
viii. Taarifa ya uwekezaji unaokusudiwa katika kuendeleza biashara ya uhifadhi na uendeshaji ghala kitaalam; na
ix. Maombi yaonyeshe aina ya mazao ambayo yanayotarajiwa kusimamiwa pamoja na mikoa husika.

Taarifa hizi ziwasilishwe kupitia barua pepe:

**Kichwa cha Habari** : **Zabuni ya kuendesha maghala ya mazao ya kilimo**
**Anuani**: info@wrrb.go.tz, **nakala itumwe** ushirika@ushirika.go.tz.

**Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe 25/04/2025.**

**Imetolewa na**